

# JARIDA LA MANISPAA YA *ya* KINONDONI

ISSN 2507-797X Toleo No 1, 2023/2024



*Uongozi makini ni tunu ya taifa letu*

TUWALINDE WATOTO WETU



**KILA LA KHERI GRADE VII 2023**

**KINONDONI**

*Kinondoni Tunajali Elimu*

**KARIBU** KUWEKEZA **KINONDONI**

## MHARIRI MKUU
Aquilinus Shiduki

## MHARIRI MSAIDIZI
Beatha Singano

## MPIGA PICHA
Kaunga Maulid

## MSANIFU WA JARIDA
Beatha Singano

## JARIDA HILI LIMETOLEWA NA
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni
S.L.P 31902 KINONDONI, DSM
SIMU: +255222170173
NUKUSHI: +255222170173
BARUA PEPE: ***md@kinondonimc.go.tz***

# RAIS MWINYI AIPONGEZA MANISPA A YA KINONDONI








**Na**
**ATHUMAN NTAFUMILA**

Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameipongeza Manispaa ya Kinondoni kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika kuwekeza ndani ya Manispaa.

Mhe. Dkt. Mwinyi amesema hayo katika hafla ya uwekaji wa jiwa la msingi katika jengo la Taasisi ya Benjamini William Mkapa liitwalo “Mkapa Health Plaza”.

“Nichukue nafasi hii kuipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa kuona na kutambua mchango wa taasisi binafsi kuja kuwekeza kwa manufaa ya wananchi wa Wilaya ya Kinondoni na Taifa kwa ujumla,” amesema Dkt. Mwinyi.

Sambamba na hayo pia Dkt. Mwinyi ameiomba taasisi hiyo kumaliza haraka ujenzi huo ili huduma za kimatibabu zianze kuwanufaisha wanakinondoni na taifa zima.

Katika hafla hiyo ilihuduria viongozi mbalimbali kutoka Manispaa ya Kinondoni wakiongozwa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza.

# KINONDONI IMEKUZA MTANDAO WA BIASHARA KWA WAJASIRIAMALI

**Na**
**JAMILA MDEMU**



Kilimo Mjini



KI
NO
NDO
NI

Uvuvi Mjini



Ufugaji Mjini



Ujasiriamali



Fursa zitolewazo na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekuwa ni chachu ya mafanikio Kwa vijana wengi.

Agnes Mnuo ni mjasiriamali anayewakilisha kikundi cha VAA Orijino Products wanaojishugulisha na uzalishaji wa bidhaa za ngozi na kutoa elimu juu ya matumizi ya bidhaa za ngozi.

Akizungumza katika maonesho ya wakulima NaneNane anasema, "kupitia mkopo wa asilimia 10 kutoka Manispaa ya Kinondoni tumeweza kutengeneza mtandao mkubwa, tumepanua masoko, tunapata wateja wa kutosha, tumeweza kuongeza uzalishaji na kuagiza bidhaa za kutosha".

Bi Agnes ameongeza kuwa, Manispaa ya Kinondoni iliwapa vijana mafunzo katika mkoa wa Kigoma ambapo mafunzo hayo yaliwapa elimu ya kutosha na kuwakutanisha na wajasiriamali wengine hivyo iliyopekekea kupata mtandao mkubwa zaidi.

Aidha, ameongeza kuwa kabla ya fursa kutoka Manispaa ya Kinondoni walikua wanatengeneza bidhaa

***Kutoka Uk....3***

chache lakini mkopo wa asilimia 10 umewakuza na kutengeneza viatu vya shule, viatu wa wazi (sandles), mabegi, mikanda, Buti, walleti, mikoba na viatu vya ofisini.

"Tunashukuru Kwa sasa tunapata oda kubwa kutoka sehemu mbalimbali na tumetambulika Kwa kiasi kikubwa".

Matarajio ya kikundi hiki ni kuwa na kiwanda kikubwa, kuongeza uzalishaji, kuwa na matawi nje ya Mkoa na bidhaa ziende nje ya nchi kwa ajili ya kujitangaza zaidi.

Kauli Mbiu "Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya chakula.

## USHIRIKANO WA MANISPAA NI NGUZO MUHIMU KWA WAJASIRIMALI

**Na**
**JAMILA MDEMU**

Ufugaji wa mbuzi wa maziwa ni teknolojia inayovutia watu wengi katika banda la Manispaa ya Kinondoni katika maonesho ya Wakulima-NaneNane. yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu J.K Nyerere Mkoani Morogoro.

Akizungumza katika maonesho hayo Bi Catherine Makabwa amesema ufugaji wa mbuzi wa maziwa umempa fursa ya kushiriki maonesho ya NaneNane kupitia banda la Manispaa ya Kinondoni.

"Manispaa ya Kinondoni imenikutanisha na wajasiriamali, nimepata elimu ya kutosha, nimepata wateja, mapokeo ya bidhaa za mbuzi yamekua makubwa" amesema Bi. Catherine.



***Moja ya mabanda ya Mbuzi wa kisasa kutoka Manispaa ya Kinondoni wanaofugwa kisasa.***

Ameongeza kuwa kupitia maonesho hayo soko litapanuka, kampuni itakua, anategemea kupata mrejesho kuhusiana na bidhaa za mbuzi ili aweze kukua zaidi kibiashara.

Aidha, Bi. Catherine amesea kupitia maonesho hayo amejifunza ukarimu, upendo, ushirikano kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. "Uongozi wa Manispaa ya Kinondoni unatoa mafunzo ya kutosha na kutamani kila mjasiriamali afanikiwe kibiashara".




*Waheshimiwa Madiwani kutoka Manispaa ya Kinondoni wakiwa katika maonesho ya NANENANE Mkoani Morogoro*







***"Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula"***

# TAHARIRI

## KINONDONI YAFANA NANENANE

Moja ya mafanikio kwa Manispaa ya Kinondoni katika maonesho ya Nanenane kwa mwaka 2023, ni kuweza kutoa mshindi wa kwanza katika Sekta ya Mifugo na kupata nafasi ya Tatu katika ushindi wa jumla.

Maonesho ya nanenane yaliyofungwa rasmi na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mheshimiwa Waziri Kindamba, yameamsha ari Mpya ya ushiriki shindani ndani ya washiriki kutoka Manispaa ya Kinondoni. Ari hii Mpya ya ushiriki wenye ushindi inachagizwa zaidi na namna Uongozi wa Manispaa na Wilaya ya Kinondoni ukiongozwa na Mstahiki Meya, Mheshimiwa Songoro Mnyonge, Mkurugenzi wa Manispaa, Bi. Hanifa Suleiman Hamza, Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Saad Mtambule na Katibu Tawala wa Wilaya, Bi. Stella Msofe, ulivyoweza kutoa Hamasa tangu mwanzo wa maandalizi hadi siku ya kilele.

Kwa upande wao, licha ya washiriki kunufaika kwa kuonesha bidhaa zao mbalimbali, ushiriki huu pia umetanua wigo wa soko la bidhaa zao ndani na nje ya Manispaa ya Kinondoni. Ushiriki wao pia umewapa washiriki hao nafasi nyingine ya kubadilishana uzoefu katika uzalishaji, uchakataji na utafutaji wa masoko.

Kwa upande wa Kilimo, Kinondoni iliweza kupeleka katika maonesho hayo mkakati maalum wa Kilimo Mjini. Kilimo Mjini, ambacho ni Aina ya kilimo kinachotumia mbinu za kisasa kwa kutumia eneo dogo na teknolojia za kisasa kinaleta tija zaidi kwa wakazi wa mjini. Hata hivyo, maonesho Hayo yamebainisha kuwa si tu Kilimo Mjini kina tija kwa wakazi wa mijini, bali hata kwa wakazi wa maeneo ya vijijini.

Sekta ya Uvuvi, nayo ilifanya vizuri katika maonesho hayo. Ufugaji wa Samaki kwa kutumia teknolojia ya kisasa na rahisi umeweza kutoa somo kwa viongozi na wananchi waliotembelea banda la Kinondoni namna bora na yenye tija ya ufugaji wa Samaki.

Sambamba na Kilimo, Ufugaji, na ushirika kupitia kwa wajasiriamali, maonesho haya pia yalitoa elimu kuhusua ufugaji bora wa mifugo hususan Mbuzi ambao licha ya kuzoea kupata mazao yake makuu ya nyama, ngozi na maziwa; ufugaji huu kupitia maonesho hayo umetoa elimu ya uzalishaji wa sabuni zitokanazo na maziwa.

Sabuni hizi zimeelezewa kuwa bora bila kuathiri afya za watumiaji.

Ni hakika, maonesho ya mwaka huu ya Nanenane yameamsha ari ya ushiriki wenye kushinda katika msimu ujao. Wahenga wanasema, kumalizika kwa msimu wa kilimo ndiyo mwanzo wa maandalizi ya msimu ujao. Tukutane Morogoro 2024.



*Moja ya matukio katika picha ikimuonesha Katibu Tawala wa Wilaya ya Kinondoni Bi, Stella Msofe, Mstahiki Meya wa Manispaa Mhe. Songoro Mnyonge pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamnza wakiwa wameshika Ngao ya Ushindi wa maenesho ya NANENANE yaliyofanyika Mkoani Morogoro 2023.*





# NMB KARIBUNI KINONDONI



*Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza akipokea zawadi kutoka kwa watumishi wa Benko ya NMB. Ikiwa ni ishara ya umoja na ushirikiano baina ya benki ya NMB na Manispaa ya Kinondoni kwa muda mrefu.*

**Na AQUILINUS SHIDUKI**

Mkurugenzu wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza ameikaribisha Benki ya NMB kuendelea kuja kuwekeza ndani hya Manispaa ya Kinondoni.

Bi. Hanifa Ameyasema hayowakati wa ziara ya Meneja wa Benki ya NMB tawi la Magomeni kuja kutoa shukrani kwa Manispaa kama mdau namba moja kwa muda mrefu.

“Hivi karibuni tumejenga vyumba vingi vya madarasa lakini bado tuna changamoto kubwa ya upungufu wa madawati hivyo nitafurahi sana iwapo NMB mtatusaidia kupata madawati kama 1500 kabla ya mwezi Disemba,’ amesema Bi. Hanifa.

Aidha, Benki hiyo imeshauriwa kutembelea jengo la Manispaa ya Kinondoni lililopo Mwenge kwa ajili ya uwekaji matangazo ya kibishara ili kujitangaza zaidi na zaidi.

Kwa upande wake Mchumi wa Manispaa ya Kinondoni Bw. Jabiri Chilumba ameishauri Bnki hiyo kuwa na madarasa ya mfano ya kufundishia kupitia teknolojia ya TEHAMA kutokan na mabadiliko ya kiteknolojia kadri yanavyokwenda’

“Ni vyema mkawa na theater za mfano ambazo zitakuwa zinatumika katika kufundishia watu angalau katika shule zetu za Msingi na Sekondari kwani hii itachangia kwa kiasi kikubwa kijipambanua zaidi kama benki,” amesema Bw. Jabir.

Kwa upande wa uongozi wa benki hiyo umeahidi kushughulikia maombi na mapendekezo yote yaliyotolewa na Manispaaya Kinondoni haraka iwezekanavyo.

Aidha benki ya NMB imeendelea kuishukuru Manispaa ya Kinondoni kwa kuendeleza ushirikiano baina yao na Manispaa kwa muda mrefu sasa.

“Tunaishuru Manispaa ya Kinondoni kwa kuendelea kutuamini na kutumia huduma zetu kwani ushirikiano wetu huu unatufanya tuendelee kuimarika zaidi na zaidi katika ktoa huduma zetu mbalimbali,” walisema.



# HONGERENI KINONDONI KWA UBUNIFU WA BIDHAA ZENYE TIJA

**Na**
**JAMILA MDEMU**



Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imepongezwa kwa ubunifu wa bidhaa zenye tija hasa katika ushindani wa kibiashara na uuzaji wa bidhaa hizo.

Pongezi hizo zimetolewa leo tarehe 03/08/2023 na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Saad Mtambule wakati akitembelea banda la Manispaa ya Kinondoni katika maonesho ya NaneNane yanayoendelea Mkoani Morogoro mapema leo hii.

"Maonesho ya mwaka huu yamekua tofauti na miaka mingine kwani kumekuwa na ubunifu wa hali ya juu, wadau wamejiandaa vizuri na wana ufahamu wa kutosha kuhusu bidhaa zao na wamekuwa na ubunifu Mkoani," amesema Mhe. Mtambule.

Aidha Mkuu wa Wilaya huyo amesema, wadau waendelee kuongeza ubunifu ili kuongeza thamani ya bidhaa kwa lengo la kuongeza kupanua masoko, kuongeza uzalishaji, kuondoa tatizo la chakula na kuongeza fursa za ajira.



Aidha Mhe Mtambule amesema, maonesho hayo yametoa elimu ya kwamba fursa moja inaweza zalisha fursa nyingine kwa kutolea mfano ufugaji wa mbuzi wa maziwa na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa ambao unazalisha maziwa, bidhaa za maziwa (sabuni), gesi ya kupikia kupitia mbolea na ajira kupitia ufugaji huo.

Vile vile,Mhe. Mtambule amesisitiza kuwa Kinondoni iwe na maonesho endelevu ili kukuza teknolojia na kutoa elimu kuhusiana na kilimo, ufugaji na uvuvi.

Kauli Mbiu ya maonesho ya NaneNane 2023 ni "Vijana na Wananwake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula".

# GREEN HOUSE NI TEKNOLOJIA BORA YA KILIMO MJINI



**Na JAMILA MDEMU**

Green House ni Kilimo bora na sahihi katika utunzaji wa mazingira na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa mjini.

Hayo yamebainishwa na John Malecela mmoja wa wakulima anayejishughulisha na kilimo cha mazao ya viungo ikiwemo karoti, nyanza, vitunguu na giligilani kwa kutumia Teknolojia mpya ya Kilimo mjini.

"Nimeamua kijihusisha na kilimo kinachotumia baada ya kugundua mazao ya viungo yana umuhimu katika kuleta ladha kwenya vyaakula mbalimbali tunavyokula," amesema John.

Aidha Bw. John amesema kuwa mapokeo katika soko ni makubwa kwani watu wengi wanapenda mazao hayo na yanatumika kila siku katika chakula.

Ameongeza kuwa, uzalishaji ni mkubwa nusu ekari inatoa matenga 300 ya nyanya na hununuliwa zikiwa shambani.

Bw. John ameongeza kuwa kafaidika na maonesho ya wakulima kwa kujifunza kuhusiana na teknolojia ya umwagiliaji wa matone, matumizi sahihi ya mbolea ya mboji na utumiaji wa dawa za asili.

Kwauoande wake Bw. Stanlaus John, jinsi ushiriki wake kwenye maonesho ya NaneNane yalivyomsaidia kupata fursa ikiwemo elimu kuhusiana na teknolojia mpya ya kilimo pasipo kutumia udongo, namna bora ya utumiaji wa dawa zinazohusiana na na kuua wadudu au kukinga mmea usiathirike (viwatilifu), kujuana na watu tofauti, na kupata masoko.

Vilevile,Bw.Stanslausi amesema elimu ya kilimo bila kutumia udongo imekuwa kivutio kwa wadau wengi katika banda hilo ambapo Bw. Evody Godrian anaelezea kuwa huzalisha mimea ya salad nyekundu na kijani ambayo soko lake kubwa ni katika Hoel na Supermarket.

"Kilimo hiki masoko yake ni mazuri kikubwa ni elimu iendelee kutolewa ili jamii ijue umuhimu wa matumizi ya salad kwenye jamii kwani wateja wengi sio watanzania".

Maonesho ya NaneNane yamekuwa na faida kubwa kwa kupata wadau wanahitaji elimu ya jinsi ya kuendesha kilimo na hii itapelekea kukua kwa sekta ya kilimo.

Kauli Mbiu ya maonesho haya ni "Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula"



# KINONDONI YATOA MAFUNZO YA USHIRIKI WA VIKAO KWA WATOTO








**Na SAUMA MWANSHULI**

Wanafunzi mbalimbali kutoka shule za Manispaa ya Kinondoni wamepewa mafunzo ya ushiriki wa vikao vya mpango wa fursa na vikwazo kwa maendeleo "O and OD".

Mafunzo hayo yametolewa leo tarehe 15. 7. 2023 ikiwa ni muendelezo wa mafunzo ya uwajibikaji wa jamii unaozingatia haki za watoto kwenye Kata na Mitaa yao.

Akiongea katika mafunzo hayo Mchumi kutoka Manispaa ya Kinondoni Bw.Bakari Mlanzi amesema nafunzo hayo yatasaidia kwa kiasi kikubwa watoto kuwa sehemu ya bajeti ya serikali.

Lakini pia muwezeshaji kutoka Shirika la Save the Chidren Bw. Alex Enock ameelezea namna jamii inavotakiwa kuwajibika katika kusimamia haki za mtoto na kuhakikisha kila kinachopangwa kwa ajili ya kuwasilisha katika serikali hakiwabagui Watoto kwa mujibu wa kanuni.

Ikumbukwe kuwa mafunzo haya ni muja ya muendelezo wa mafunzo kwa wanafunzi wote kutoka shule zote za Manispaa ya Kinondoni ndani ya Kata 20.

Mafunzo hayo yatasaidia kwa kiasi kikubwa katika kutimiza utekelezaji wa mahitaji na haki za watoto ndani ya Manispaa ya Kinondoni kwa mujibu wa sheria zilizowekwa.

# MFUMO WA UCHAKATAJI MAJI TAKA NI RAFIKI WA MAZINGIRA KINONDONI

**Na**
**KMC Online Media**




Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekaa kikao cha kutambulisha Mradi wa Kuchakata Maji Taka katika Kata ya Kawe na Kunduchi.

Mradi huo utahusiana na mfumo wa kutoa maji machafu majumbani kupeleka kwenye mfumo wa kuchakata maji taka ili kuondoa sumu na kuweza kuyatumia maji hayo katika matumizi mengine ikiwemo umwagiliaji wa mashamba.

Kikao hicho kimefanayika leo tarehe 19 Julai, 2023 na kukutanisha wadau mbalimbali wa maendeleo wakiwepo watumishi wa umma, walimu wakuu, viongozi wa chama tawala CCM, viongozi wa ngazi ya mtaa pamoja na ngazi ya Kata.

Mradi huu utasimamiwa na DAWASA na kiasi kilichotetengwa kukamilisha mradi huu ni jumla ya shilingi 52, 407,401,647.15.

Wadau mbalimbali wameeleza umuhimu wa mradi huo kuwa utapunguza gharama za kunyonya maji machafu , kuondoa kero za uchafuzi wa mazingira, kuondoa mazalia ya mbu, kuleta ajira, na kuondoa magonjwa ya mlipuko.

Akiongea muwakilishi wa Mbunge wa kawe Bw. Juma Adam amesema Mkandarasi anatakiwa kukabidhi ramani hadharani wananchi wajue kinachotarajiwa kufanyika na kusisitiza kupanga ratiba vizuri na viongozi wa Mtaa Ili mradi ufanikiwe ipasavyo.

Vilevile Katibu Mwenezi wa CCM Bw. Potipoti Ndanga amesisitiza suala la ushirikiano na viongozi wa Mtaa ili kufanikisha zoezi hilo.

Ameongeza kuwa " Elimu itolewe kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, viongozi wa dini na kuandaa matamasha ya kuhamasisha zoezi hilo".

Amesisitiza fursa ya ajira kwenye mradi huo itolewe kwa wazawa ili kupata ushirikiano pindi wapitapo majumbani wakati wa zoezi hilo.





# MAKALA ZETU
# KIVYETU VYETU






**Kinondoni ni Sehemu Sahihi na Salama kwa Uwekezaji**





**Miundombinu bora, Afya bora, Elimu bora kwa Ustawi wa Manispaa ya Kinondoni**

# KINONDONI YAFIKIA ASILIMIA97 MAKUSANYO YA MWAKA 2022/2023

**Na KAUNGA MAULID**



Naibu Meya Manispaa ya Kinondoni, Mheshimiwa Joseph Rwegasira, amempongeza Mkurugenzi Bi. Hanifa Suleiman Hamza, kwa kufanikiwa kukusanya zaidi ya Shilingi bilioni 54.5 kati ya bilioni 57.2 zilizopangwa kukusanywa kama mapato ya ndani kwa mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 93 ya lengo.

Mhe. Rwegasira ametoa pongezi hizo wakati akiwasilisha taarifa ya Robo ya Nne kwa mwaka 2022/2023 katika Baraza la Madiwani lililoketi hivi karibuni. "Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi na uongozi mzima wa Manispaa ya Kinondoni kwa ukusanyaji wa fedha kwa asilimia 93 ndani ya mwaka huu ikiwa ni sawa na lengo tulilokusudia," amesema Mhe. Rwegasira.

Jumla kuu ya bajeti ilikuwa Shilingi bilioni 131 ikijumuisha bilioni 1.1 matumizi mengineyo (other charges), bilioni 54 kwa ajiri ya mishahara na bilioni 14 kwa ajiri ya miradi ya maendeleo.

Kwa upande wake, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mhe. Songoro Mnyonge, amesisitiza fedha zilizotengwa kwa ajiri ya utekelezaji wa miradi mbalimbali inafanyika kama ilivyopangwa. "Natoa rai kwa fedha zote ambazo ni asilimia 70 zilizotengwa kwa ajiri ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2022/2023 zitumike kama ilivyopangwa" amesema Mhe. Songoro.

Mhe. Songoro amesema kuwa moja ya mambo ambayo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondi imekuwa ikijivunia ni uwekezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ndani ya Manispaa hivyo usimamizi na utekelezaji ni jukumu la kila mtu. Katika pongezi hizo, Mshemiwa Songorro ameungana na Mheshimiwa Rwegasira kwa kusema, "Wanasema mnyonge mnyongeeni ila haki yake mpeni, sina shaka na uongozi wa Mkurugenzi napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa niaba ya Madiwani wote hivyo apewe maua yake."

Ukusanyaji wa mapato kwa kiwango kikubwa unatoa dira na mwanga mkubwa katika kuleta maendeleo ndani ya Manispaa ya Kinondoni kwani fedha iliyokusanywa kama pato la ndani zitaenda kutekeleza miradi kutoka sekta mbalimbali ikiwepo sekta ya Afya, Elimu, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Michezo, Utamaduni na Sanaa.

***Naibu Meya na Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI Manispaa ya Kinondoni Mheshimiwa joseph Rwegasira kiwasilisha taarifa ya Robo ya Nne kwa mwaka 2022/2023 katika Baraza la Madiwani Manispaa ya Kinondoni lililoketi hivi karibuni.***

# MATUKIO KATIKA PICHA













# LTIP KUKWAMUA URASIMISHAJI KINONDONI

**Na AQUILINUS SHIDUKI**



Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Bi Hanifa Suleiman Hamza leo amemshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuleta Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi wenye lengo la kuwezesha usalama wa ardhi kwa watanzania wote.

Bi. Hanifa alitoa shukrani hizo wakati wa kuutambulisha rasmi mradi huo katika ngazi za Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam ambapo alisema “utatatua changamoto nyingi za Urasimishaji ndani ya Manispaa.”

Mtaalam Muwakilishi wa Mradi huo kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Bi. Aisha Masanja, alielezea kuwa, “kupitia Ardhi Kliniki katika ngazi za Mitaa, mradi utaanza kwa kutoa hati papo hapo, kumalizia kazi za upangaji na upimaji ardhi zilizokwama awamu ya kwanza kupitia Mpango wa Ukwamuaji Urasimishaji Mkoa wa Dar es Salaam.” Bi. Aisha aliongeza kuwa mradi huo utajenga uelewa wa pamoja ili kutekeleza vyema mpango wa ukwamuaji urasimiashaji kwa Manispaa ya Kinondoni.

# KINONDONI YAZIDI KUIMARISHA SEKTA YA AFYA KWA KASI

**Na SAUMA MWANSHULI**




Sekta ya Afya ndani ya Manispaa ya Kinondoni imezidi kuimarika katika kipindi cha mwaka 2022/2023.

Taarifa ya Utendaji na Uwajibikaji ya Divisheni ya Afya, imebainisha maeneo yanayoonekana kung’ara kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa huduma za chanjo kwa kina mama wajawazito na watoto chini ya miaka 15, ambapo takliban watoto chini ya miaka mitano 41,416 wamepatiwa chanjo.

Aidha, taarifa inaeleza kuwa, “jumla ya rufaa 2,886 zimetolewa kwa akina mama wajawazito na watoto ambazo zimesaidia kupungua kwa idadi ya vifo kwa akina mama na watoto kutoka 19 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufika vifo 16 na kupungua kwa vifo vya watoto wachanga kutoka 546 hadi kufikia vifo 454.”

**Ujenzi wa vituo vipya vya Afya**

Halmashauri imeendelea na ujenzi wa vituo vipya vya Afya katika maeneo ambayop hayakuwa na huduma hiyo ili kusogeza huduma kwa wananchi. Vituo hivyo ni Malindi Estate, Ally Maua na Nyakasangwe ambavyo kwa sasa vinatoa huduma. Wakati majengo mengine ya maabara, mionzi na huduma za dharura katika Hospitali ya Wilaya iliyopo Mabwepande; huko Mbopo ukarabati na upanuzi wa jengo la wagonjwa wa nje, wazazi, nyumba Mbili za watumishi pamoja na Zahanati ya Mbopo unaendelea ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma.

Taarifa inabainisha kuwa, “Vilevile upanuzi wa Zahanati ya Kawe kuwa kituo cha Afya na kuongeza majengo ili kuboresha huduma zitolewazo kwa wananchi ambapo mpaka sasa majengo ya maabara, wazazi, upasuaji na kichomea cha taka vimekamilika na kuanza kutoa huduma.”

# KITUO CHA DALADALA MWENGE KIMEFIKIA PAZURI



## Na KMC MEDIA

Mradi wa umaliziaji wa kituo cha kisasa cha Daladala eneo la Mwenge kilichopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni utasaidia kutatua changamoto za usafiri kwa kusogeza huduma za usafirishaji, kuboresha na kuweka mazingira mazuri ya miundombinu kwa jamii.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni katika kuboresha huduma za jamii kwa wananchi na wafanyabiashara wa eneo la Mwenge na Wilaya kwa ujumla iliamua kuanzisha ujenzi wa kituo cha mabasi Mwenge kwa fedha za mapato ya ndani katika mwaka wa fedha 2019/2020-2022/2023.

Mradi wa kituo cha mabasi Mwenge unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza mradi ulitekelezwa kwa Force Account chini ya Local Fundi kikosi cha jeshi la wananchi Na. 361 Rejimenti kwa gharama ya Tshs 7,033,575,688.00 gharama iliyotumika mpaka mradi unasimamishwa ni Tshs 1,905,373,174.43.

Awamu ya pili Halmashauri iliingia mkataba na Mkandarasi HEINAN INTERNATIONAL LTD ambaye ndiye mjenzi kwa gharama ya Tshs 9,810,000,000 na msimamizi wa mradi huu akiwa na mhandisi mshauri "CRYSTAL CONSULTANTS" kwa gharama ya Tshs 304,136,064.00.

Utekelezaji umefikia asilimia 87 ambapo kazi zinazofanyika kwa sasa kwenye jingo la maduka na car dervice ni umalizaji (skimming, kuweka ceiling boards, tiles na kuweka frem za madirisha). Jengo la msikiti kazi imekamilika. Kituo cha manasi kazi ya kuweka bays na kutengeneza barabara ya kutokea inaendelea.

Mksndarasi kalipwa pesa ya malipo kwa asilimia 26 ambayo ni Tshs 2,591,648,597.72. Na malipo yaliyofanyika kwa Mhandisi mshauri ni Tshs 304,136,064.00 na mpaka sasa mradi huu umetumia jumla ya Tshs 4,801,157,835.72

Katika kukamilisha mradi huu kituo kitakua na majengo matatu ambayo ni jingo la biashara lenye sakafu tatu litakalokuwa na jumla ya maduka 128 kwa ajili ya wafanyabiashara, vyumba 11vitakavyoyumika kama ofisiza kukodi, vyumba 12 kwa ajili ya mama lishe, migahawa ya chakula miwili, duka la kuuza vyakula (min supermarket) moja na vyoo kila sakafu.

Pia kuna jengo la kuhudumia magari (car service) ambalo litakuwa na sehemu ya kutengenezea magari na bajaji pamoja na maduka mawili ya vifaa vya magari (spare parts).

Jengo la walinzi ni ni mojawapo ya moango wa mradi huu.

Licha ya kuwepo kwa majengo haya pia kuna mpango wa kuwepo kisima cha kuhifadhia maji safi (underground water tank) chenye uwezo wa lita za ujazo 70,000.00 (70m3)

Mradi huu utajenga kituo cha mabasi ambacho kina uwezo wa kuhudumia madaladala 100 kwa wakati mmoja, magari binafsi 85 na bajaji 60.

Mradi wa mbolea ya asili katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ni muhimu katika jitihada za kusaidia usafi wa jiji na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na ni matarajio ya Manispaa kuwa na mikakati endelevu ya mradi huu kwa ajili ya manufaa ya Manispaa na wananchi wa jiji la Dar es slaam kwa ujumla.

Mradi huu wa umaliziaji wa kituo cha kisasa cha mabasi Mwenge kitasaidia kuongezaya HalmashauriyaMAnispaa ya Kinondoni (mradi unaotajiwa kuingiza Manispaa shilingi 800,000,000.00 kwa mwaka utakapokamilika.

# DC MTAMBULE AZINDUA MRADI WA BOOST WENYE THAMANI YA Tsh. BILIONI 1.5




*Mkuu wa Wilaya Mhe. Saad Mtambule (kushoto) akikata utepe katika uzinduzi wa mradi BOOST katika shule ya Ali Hassan Mwinyi huku akimbatana na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza (kulia) na Diwani wa Kata ya Magomeni Mhe. Nurdin Yusuph (kulia).*

**Na JAMILA MDEMU**

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni,, Mheshimiwa Saad Mtambule, hivi karibuni amezindua miradi ya Boost yenye thamani ya shilingi 1,522,100,000.

Miradi hiyo imehusisha wa ujenzi wa madarasa, matundu ya vyoo, vichomea taka, katika shule ya Msingi Ali Hassani Mwinyi, Mapinduzi, Kunduchi, Kisauke, Mkwawa, Mchangani na Mtambani.

Katika uzinduzi huo uliofanyika Shule ya Msingi Ally Hasan Mwinyi Mheshimiwa Mtambule alimpongeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Bi. Hanifa Suleiman Hamza kwa usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo hadi kukamilika kwake. “Nakupongeza Mkurugenzi kwa kufuatilia kwa ukaribu miradi hii kwani, kwa kufanya hivyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kukamilika kwa kabla ya wakati uliopangwa”. Amesema Mhe Mtambule.

Naye, Bi. Hanifa alimweleza Mkuu wa wilaya kuwa katika fedha iliyotengwa mwaka 2022/2023 Kinondoni imefanikiwa kujenga vyumba vya madarasa 51, matundu ya vyoo 66, majengo ya utawala 2 na vichomeo taka viwili ambavyo vimekamilika.

Pia Bi. Hanifa amewasisitiza wanufaika wa miradi hiyo kuitunza. “Kinondoni imekuwa ya kwanza katika wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam kukamilisha miradi hii, niwaombe walimu na wanafunzi kuwa mstari wa mbele katika kutunza miundombinu hii ili iweze kusaidia vizazi vijavyo”.

- Madawati 535 Yasambazwa Kinondoni

Katika kukabiliana na upungufu wa madawati shuleni, jumla ya madawati 535 yamesambazwa katika shule 12 za Manispaa ya Kinondoni kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mwaka wa utendaji kazi ya mwaka 2022/2023 Shule zilizonufaika huku idadi ya madawati ikionekana kwenye mabano ni Kunduchi (105), Ununo (36), Bunju A (50), Lugalo (75), Mikumi (20), Mzimuni (24) na Mwananyamala Kisiwani (38). Shule nyingine ni Mwangaza (23), Mapinduzi (33), Wazo Hill (40) na Mikocheni (60)

- Tandale Kupata Sekondari ya Kata

Wakati mchakato wa kuipatia Tandale sekondari ya Kata ikiendelea ili kutimiza kata zote 20 kuwa na sekondari, hivi karibuni Manispaa imetenga zaidi ya shilingi Milioni 600 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa 24 katika shule za sekondari zikiwemo Boko Mtambani, Godwini Gondwe na shule Kumbukumbu.

Aidha, katika kipindi hicho, taarifa inaeleza kuwa, “miradi ya Ujenzi wa Maabara kwa shule ya Sekondari za Kijitonyama Sayansi, Daniel Chongolo, Magomeni Makuti, Boko Mtambani na Mikocheni Sekondari unaendelea kukamilishwa kwa kupelekea fedha za mapato za ndani.

# KINONDONI IMEJENGA VYUMBA VIPYA VYA MADARA 51 2022/2023

**Na KMC MEDIA**

Mwaka 2022/2023 Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imefanikiwa kujenga vyumba vya madarasa 51, matundu ya vyoo 66, majengo ya utawala 2 na vichomeo taka viwili ambavyo vimekamilika.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mwaka wa utendaji kazi ya mwaka 2022/2023 Manispaa ya Kinondoni imefanikiwa kuongeza idadi ya madawati katika shule 12.

Moja ya shule zilizonufaika ni pamoja na Shule ya Msingi Kunduchi (105), Ununo (36), Bunju A (50), Lugalo (75), Mikumi (20), Mzimuni (24) na Mwananyamala Kisiwani (38). Shule nyingine ni Mwangaza (23), Mapinduzi (33), Wazo Hill (40) na Mikocheni (60)

Ikumbukwe kuwa wakati mchakato wa kuipatia Tandale sekondari ya Kata ikiendelea ili kutimiza kata zote 20 kuwa na sekondari, hivi karibuni Manispaa imetenga zaidi ya shilingi Milioni 600 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa 24 katika shule za sekondari zikiwemo Boko Mtambani, Godwini Gondwe na shule Kumbukumbu.

Aidha, katika kipindi hicho, taarifa inaeleza kuwa, "miradi ya Ujenzi wa Maabara kwa shule ya Sekondari za Kijitonyama Sayansi, Daniel Chongolo, Magomeni Makuti, Boko Mtambani na Mikocheni Sekondari unaendelea kukamilishwa kwa kupelekea fedha za mapato za ndani.







# TUNA IMANI NA KASI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YETU

## *Kinondoni Tunajivunia na Kasi ya Miradi ya Maendeleo*

Moja ya mikakati mikubwa ya kuimarisha na kukuza maendeleo ndani ya Manispaa ya Kinondoni ni kukagua na kusimamia iapasavyo kasi ya utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo inaendelea kutekekelezwa kwa kasi, Binafsi kama Manispaa ya Kinondoni tunapenda kumshukuru Rais Dkt, Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha ili tuweke kutekeleza baadhi ya miradi hasa katika sekta ya elimu na afya.

Wanakinondoni tunasema asante mama kwa kutuletea fedha hizo.



# TANGAZO

**Kuelekea siku ya maadhimisho ya chanjo ya kichaa cha Mbwa Kitaifa, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inapenda kuwakaribisha wamiliki na wafugaji wote wa Mbwa kuwaleta Mbwa wao kupata chanjo kuanzia tarehe 27 - 28 September 2023**

**Kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 11:00 Jioni**

**Kata ya Bunju**





# KMC MICHEZO



## MSIMU HUU 2023/2024 KMC NI ZAMU YETU




## KINO BOYS

Kikosi cha KMC FC kinaendelea kujinoa dhidi ya michezo inayofuata katika Ligi Kuu Tanzania Bara ya NBC.

KMC FC inatarajia kushuka dimbani mnamo Septemba 15 kukipiga dhidi ya JKT Tanzania katika uwanja wa Uhuru.

Baada ya mchezo huo KMC FC itashuka dimbani Septemba 30 dhidi ya Geita Gold katika uwanja Nyankumbu.

Hadi sasa Kmc fc imecheza jumla ya mechi mbili ambapo imepoteza mchezo mmoja na kutoa sare mchezo mmoja.

Kwasasa KMC FC ipo nafasi ya 14 ikiwa na alama 1

## WAACHE WAJE



# UWANJA MPYA WA MPIRA UTAHAMASISHA UKUZAJI WA VIPAJI VYA MICHEZO



## Na KMC MEDIA

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekusudia kujenga mradi wa ujenzi wa uwanja wa mpira katika mtaa wa Mwenge ili kukuza vipaji vya michezo, kutoa ajira kwa jamii, kuongeza mapato ya serikali na kupanga wigo wa biashara kwa wananchi.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ni miongoni mwa Manispaa inayofanya vizuri katika kila sekta kama uchumi, afya ikiwemo sekta ya michezo ambayo imepelekea Kinondoni kujulikana katika mikoa mingi nchini Tanzania.

Mchezo wa mpira wa miguu unatokana na kuwepo kwa timu ya KMC FC inayoshiriki ligi kuu soka Tanzania bara umepelekea Manispaa ya Kinondoni kufanikiwa katika kila nyanja ikiwemo kiuchumi, kijamii na hata kiafya.

Mradi huu wa ujenzi wa uwanja wa mpira utawakutanisha watu kutoka kata mbalimbali katika Manispaa ya Kinondoni na Manispaa nyingine jijini Dar es Salaam kushabikia michezo ikiwemo timu ya KMC FC ambayo imefanikiwa kuwa na mashabiki wengi kutoka ndani na nje ya Manispaa ya Kinondoni.

Na pia mradi huu utasaidia kutoa ajira kwa vijana ambao ni wazawa na wasio wazawa kutokana na ushindani mkubwa uliopo baina ya timu ya KMC FC na timu nyingine hivyo itaongeza ushindani mkubwa na kusaidia kuleta wawekezaji watakaokuza uchumi wa Manispaa ya Kinondoni.

Mradi huu pia utaongeza soko la vijana ambao watatumia uwanja huo kufanya mazoezi na kupelekea kushiriki kwenye michuano mbalimbali na hatimaye kupata vijana wenye uwezo mkubwa katika tasnia ya michezo.

Mradi huu ni miongoni mwa miradi ya kimkakati katika Manispaa ya Kinondoni inayotekelezwa kwa fedha za ndani na umegawanyika katika sehemu mbili ambazo hutekelezwa kwa kutumia mkandarasi Group Six International na Local Fundi.

Local fundi alianza mradi huu tar 03/02/2020 hadi 02/04/2021 ambapo mradi ulisimamishwa kupisha uchaguzi na kuanza tar 20/05/2022 na alitakiwa kukamilisha mradi huo baada ya miezi 6.

Ukamilishwaji wa mradi huu utatekeleza yafuatayo; kutakuwepo na majengo yenye maduka 70, hosteli ya wachezaji yenye vyumba nane, sehemu ya kufanyia mazoezi ya viungo (GYM), majukwaa ya watu maalum (VIP) pamoja na vyoo kwa ajili ya mashabiki na wafanyabiashara watakaopanga eneo la maduka.

Mradi huu pia utasaidia kuwepo kwa uwanja na majukwaa ya kawaida yenya uwezo wa kuchukua watu 3,500.

Mradi huu utapelekea kupata visima viwili vya kuhifadhi maji vitakavyokuwa na uwezo wa kuhifadhi maji lita 30,000. Vile vile mradi utarahisisha kuwepo kwa genereta.

Aidha, hatua ya mradi umefikia asilimia 15 ambapo kazi inayoendelea kwa sasa ni uwekaji wa kifusi na kuweka sawa eneo zima na kazi ya kujenga majukwaa kwa ajili ya mashabiki.

Mradi umekamilika kwa asilimia 98 na umefika hatua ya kupaka rangi na kufunga vifaa vya umeme. Vile vile mkandarasi amelipwa malipo ya awali na yameshafanyika manunuzi ya vifaa vya ujenzi.

# JARIDA LA MANISPAA YA KINONDONI









Jarida la Manispaa ya Kinondoni 2023/2024

*www.kinondonimc.go.tz*